BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

THE TANZANIA GLOBAL DIASPORA COUNCIL (TDC GLOBAL)

KATIBA YA BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

KATIBA YA BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

Sisi wanachama wa TDC Global, tukiwa na nia ya kuunda umoja na mshikamano, ili kushirikiana na kukuza, hamasa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Nchi yetu.

Tutazidi kuimarisha mahusiano mazuri, ushirikiano katika kukuza tamaduni, shughuli za kijamii na masuala yote yanayoathiri watanzania wanaoishi ughaibuni kwa kupendekeza sera na mabadiliko ya sheria tofauti bila kuathiri ulinzi wa rasilimali za Tanzania, usalama wa taifa na umoja wetu wa kitaifa wa muda mrefu.

Ili kutimiza haya, tutashiriki katika kuchangia kutoa ufumbuzi na kuwekeza katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu kwa manufaa yetu na watu wote wa Tanzania. Baraza kupitia shughuli zake litawasaidia watanzania kwa kuhamasisha kulinda rasilimali za watanzania, na watanzania waliopo ughaibuni kuweza kuchangia ukuaji wa kiuchumi na kijamii nyumbani Tanzania, kupanua na kuimarisha mahusiano mazuri na ushirikiano na serikali ya tanzania na watu wa Tanzania kama ilivyosemwa hapo juu. Hivyo, tunaamuru kuanzishwa kwa katiba ya watanzania wanaoishi ughaibuni wanaowakilishwa na baraza la diaspora la watanzania.

MLEZI
Baraza kwa heshima litaonana na kumuomba mheshimiwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa MLEZI wa baraza la diaspora la watanzania.

UFAFANUZI
Fafanuzi zimetolewa katika kiambatanisho cha kwanza.
1. JINA
Jina la ushirika ni “BARAZA LA DIASPORA DUNIANI TANZANIA” kwa kifupi “TDC GLOBAL” na itajulikana hapa kama “Baraza”

2. TANBIHI
TDC GLOBAL ni taasisi iliyosajiliwa chini ya sheria za taasisi za Uswidi.
Litakua shirika jumuishi na kwamba:

a) Halitakua na mlengo wa chama cha kisiasa wala cha kidini;
b) Litapinga aina zote za ubaguzi; na
c) Limeundwa chini ya msingi wa taasisi zisizo na faida kifedha ili kuwakilisha na kukuza maslahi ya wanachama wake.

3. KIFUNGU CHA “KUTOKUWA TAASISI YA FAIDA”
Mali na mapato ya TDC Global vitatumika katika uendelezaji wa malengo yake, na hakuna sehemu ya mapato au mali hizo zitakaNzosambazwa kwa wanachama wa baraza hili isipokua kama fidia ya huduma zinazotolewa na gharama zilizotumika kwa niaba ya baraza.

4. USIMAMIZI YA KANUNI ZA HAKI

TDC Global itafanya kazi zake kwa kuzingatia na kusimamia matumizi ya kanuni za haki na usawa, bila kuathiri haki za kijamii katika sera zake zote, mipango, huduma, shughuli na utekelezaji wa kazi zake.

5. MAKAO MAKUU NA USAJILI

Baraza la diaspora la watanzania litasajiliwa kama ushirika nchini Uswidi chini ya uongozi wa kamati ya utendaji ya jumuiya ya watanzania Uswidi. Makao makuu ya TDC Global yatakua jijini Stockholm Uswidi. Ofisi ya utawala inaweza kuwa katika nchi nyingine yoyote kulingana na uhitaji, ufanisi na utekelezaji wa shughuli za TDC Global.

6. MAONO

Kuwa shirika lenye ustadi linalokuza maslahi ya watanzania wanaoishi ughaibuni wanapohusika katika maendeleo ya uchumi wa Tanzania na maendeleo ya ustawi wao. TDC Global itashirikiana na serikali ya Tanzania kutengenza "sera ya diaspora" inayounganisha mahitaji ya kimaendeleo ya nchi na rasilimali watu pamoja na uchumi za watanzania waishio ughaibuni.

TDC Global itakua daraja linalotambulika kati ya serikali ya Tanzania na watanzania wanaoishi ughaibuni, ikitetea na kushawishi kwa mabadiliko ya sheria za kitanzania zinazoathiri ushiriki wa watanzania walio ughaibuni kiuchumi, kijamii na kitamaduni katika shughuli za nchi. Baraza litafuatilia kuondolewa kwa vikwazo ambavyo huzuia mchango kamili wawatanzania walioko ughaibuni katika maendeleo ya Tanzania na watu wake, kwa moyo huo, TDC Global itafanya kazi na serikali ya Tanzania ili kufikia uamuzi wa serikali kutoa ruhusa kwa uraia wa nchi mbili kwa watanzania waishio ughaibuni.

Katika kutekeleza malengo yake, baraza litahusisha au kufanya kazi kwa karibu na vyombo vingine au makundi yenye maslahi na malengo sawa ikidumisha uhuru wake kama chombo cha kujitegemea.

7. MALENGO

Baraza likiwa kama kiungo kikuu cha watanzania walioko ughaibuni kupitia uwanachama binafsi, mashirika ya kijamii ya Tanzania katika nchi na uwakilishi wa taasisi za mabara tofauti. Inalenga kuleta pamoja na kuunganisha watanzania walioko ughaibuni wanaoishi katika mabara yote ya dunia ikijumuisha bara la Afrika isipokua nchi ya Tanzania. Hivyo, TDC Global itafanya yafuatayo:

a) Kuhamasisha, kuunganisha na kuwawezesha watanzania waishio ughaibuni kwa kuandaa fursa ughaibuni ya kuwasiliana na serikali ya Tanzania na kinyume chake. Ili kufanikisha lengo hili, na kwa uzingatia maslahi ya wanachama wake, baraza litafanya jitihada zifuatazo;

I. Kushirikiana na watanzania wote wanaoishi ughaibuni na kukusanya maoni yao juu ya sera na sheria zinzoathiri ushiriki na mchango wao kamili kwa maendeleo ya tanzania.

II. Kushawishi serikali ya Tanzania kwa niaba ya wanachama wake wote kuhusiana na masuala yote yenye maslahi kwao kiuchumi, kijamii na

kitamaduni ikiwa ni pamoja na kupata faida zao kama wazawa wa Tanzania kama kuruhusiwa kuwa na uraia wa nchi mbili.

III. Kutumia rasilimali watu na nyenzo za watanzania waishio ughaibuni katika kuendeleza maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni ya Tanzania.

IV. Kujenga na kuitangaza picha nzuri ya Tanzania duniani kwa lengo la kuongeza kiwango cha utalii na kufanya Tanzania kuwa chaguo la kwanza katika biashara za kimataifa na uwekezaji Afrika.

b) kukuza, kutetea na kulinda haki ya uzawa na maslahi ya kibiashara ya Tanzania, ya wajumbe wake, na hadi sasa inaweza kuwa sawa na malengo yafuatayo:

I. Kusaidia na kuhamasisha maendeleo ya biashara na uwekezaji kati ya nchi amabazo watanzania walio ughaibuni na waliopo Tanzania.

II. Kukusanya, kupata, kuchapisha na kusambaza taarifa na takwimu na maelezo mengine kuhusu mchango wa watanzania waishio ughaibuni katika biashara, uwekezaji, elimu, afya na mambo yanayohusiana nayo ambayo inaweza kuwa ya maslahi kwa wanachama wake na maendelea ya tanzania.

III. Kuandaa kongamano la kimataifa la watanzania waishio ughaibuni kila mwaka kuwezesha mazungumzo, kufuatailia maendeleo ya malengo, kuendeleza mipango ya utekelezaji na kujumuika na watu tofauti kutoka sehemu tofauti za dunia.

IV. Kukuza mahusiano ya kijamii na kiuchumi kati ya wanachama duniani kote na kati ya wananchama na wageni maarufu wenye wadhifa kutoka tanzania na maslahi husika kwa wanachama.

V. Kushirikiana na au kuwa na uhusiano na kuchangia shughuli za taasisi, jamii, vyama au kampuni zinazofuata malengo yanayofanana ambayo yanaweza kuwa ya faida kwa wanachama.

c. Kuchangia kwenye jitihada za wanachama ili kuboresha ubora wa maisha ya mtu binafsi, ulinzi wa maslahi yao, mahusiano na ushirikiano.

d. kuwezesha kuundwa kwa nafasi mpya za ajira na fursa za mafunzo tanzania kwa kuhimiza, kuhamasisha na kuwezesha wanachama wake kushiriki katika uwekezaji, biashara, utalii, kupeana ujuzi na kuongezeka utumiaji wa fedha za kigeni nchini

e. kuhamasisha wanachama kuunda mfuko wa hiari wa baraza ambao utasaidia kuchangia katika elimu, afya, huduma za ulemavu, makazi na uwepo wa chakula.

f. kuandaa shughuli za kuchangia mfuko kutoka kwa vyama vyenye nia katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ili kutimiza malengo ya shirika.

g. kuimarisha roho ya kujitolea kwa kuwa na watanzania waishio ughaibuni wanaojitolea wakiwa na mpango kazi wa muda mfupi na wa muda mrefu ili kuratibu watanzania

waishio ughaibuni kushiriki katika shughuli za dharura au utoaji wa misaada kama itakavyohitajika.

h. kukusanya na kusambaza habari, kuelimisha na kuwajulisha juu ya mambo yote yanayoathiri madhumuni ya watanzania waishio ughaibuni kupitia makusanyiko, semina, warsha, mikutano na njia nyingine za utangazaji ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari.

i. kufanya chochote au vitu vyote vinavyofaa ili kufikia malengo yaliotajwa awali.

j. kuungana na mashirika binafsi, ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali kwa niaba ya wanachama katika kufikia malengo ya TDC Global.

k. kuwapa wanachana habari kuhusu sera, taratibu zinazohusiana na fursa za uwekezaji nchini tanzania, kuwezesha ushiriki wa wanachama katika michakato ya zabuni na kuunga mkono miradi nchini tanzania.
    a. kutoa huduma za ushauri za zabuni na maendeleo ya biashara kwa wanachama kama inavyohitajika na kuwa mwakilishi kwa wale wanaotaka kuidhinisha baraza kushughulikia biashara kwa niaba yao.

l. kuandaa maonyesho ya biashara pamoja na matukio ya kijamii na kiutamaduni kusaidia kazi ya baraza na hatimaye kukuza picha nzuri ya tanzania na watanzania popote walipo.

8. MAMLAKA YA BARAZA

Kwa kufuata malengo yaliyowekwa hapo juu, baraza la diaspora la watanzania litasimamiwa na Kamati ya Utendaji iliyochaguliwa ambayo itasimamia shughuli za baraza husika.
Kamati ya Utendaji itakuwa na madaraka yote ya usimamizi wa TDC Global kwa niaba ya TDC Global; na katika mambo fulani, Kamati ya Utendaji itatumia mamlaka hayo kwa kushauriana na uongozi wa Uongozi wa timu ya TDC Global. Kamati ya Utendaji itaungwa mkono na Bodi ya Ushauri ya TDC Global. Zaidi ya hayo, Baraza lina mamlaka katika nyongeza,maondoleo na marekebisho yafuatayo :

1) Kwa kushirikiana na idara za serikali na mashirika mengine yenye uhalali na taasisi kwa ajili ya kuendeleza malengo ya Baraza;

2) Kukubali zawadi yoyote, wasia au kifaa au mali binafsi iwe kwa hali ya kuamini ya kipekee au la kwa vitu vyovyote iwe kimoja moja au zaidi kwa ajili ya baraza;

3) Kuzalisha fedha kwa njia ya michango ya umma na njia nyingine yoyote kama itakayoweza kutumika mara kwa mara na kupitishwa na Kamati ya Utendaji ndani ya sheria elekezi inayosimamia maadili ya chama. Pesa hizo zitatumika kufikia malengo ya Baraza;

4) Kununua, kuchukuliwa kwa ajili ya kukodisha au katika kuibadilisha, kukodisha au vinginevyo kupata uhalali au mali binafsi au haki zozote upendeleo ambao baraza umeafiki kwa kufikiria muhimu au unahitajika.

5) Kuuza, kubadilishana, kukopesha, kukodisha, kuondoa au kuibadili na akaunti au vinginevyo kushugulika na vyote au sehemu yoyote ya mali binafsi kuwa mali ya baraza.

6) Kuwa wajumbe wa, kujiunga na, au misingi ikiwa imeingizwa au kuwa na vitu kabisa au sehemu zinazohusiana na ustawi wa jamii ya watanzania ughaibuni au nyumbani.

7) Kukopa fedha zitakazohitajika kwa jili ya mahitaji ya baraza.

8) Kuwekeza fedha zozote za baraza husika mara moja itahitajika ikiwa na idhini ya aliyepewa mamalaka sheria ya nchi ya Sweden ili kulinda imani.

9) Kuchapisha magazeti, vipeperushi au nyaraka nyinigne au kutangaza kupitia chombo chochote au vyanzo vya habari vya elektroniki ikiwa ni sehemu ya kamati ya utendaji na uongozi wa timu itaridhia ni njia bora kukuza malengo ya baraza.

10) Kufungua na kutunza akaunti za benki yenye jina la baraza husika.

11) Kuteua, kuajiri na kulipa malipo kwa muda wote, muda maalum, muda wa kudumu, maafisa wa muda mfupi, waajiriwa na wafanyakazi wa baraza, ambapo mmoja kati yao anaweza kuwa ni Mtendaji Mkuu.

12) Kusitisha, au kufukuza kwa muda wote, muda maalum, muda wa kudumu, waajiriwa wa muda mfupi, ambapo mmoja kati yao anaweza kuwa ni Mtendaji Mkuu.

13) Kupanga, kuimarisha na kulipa malipo yoyote ya bima kwa jili ya mali zote za baraza ambapo baraza lenyewe litaridhia na kujiridhisha umuhimu wa malipo hayo kutoka kipindi kimoja cha muda hadi kipindi kingine cha muda.

14) Kuingia kwenye majadiliano, mikataba na makubaliano yanayohusisha maslahi ya baraza.

15) Kubatilisha, kutofautisha na kutekeleza vitendo vyote, shughuli na mambo yanayouhusiana na mipango ya ratiba kwa maana ya maslahi ya baraza;

16) Kufanya jambo /kitu chochote ikiwa kina umuhimu,muafaka au inaruhusu mazingira ya wajibu na malengo ya chama/shirika.

8.1 Bodi ya Ushauri ya TDC Global.

Itakuwa:

a. Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji (mjumbe mshiriki)
b. Timu ya Uongozi wa TDC Global inajengwa na:
    - Wananchama Waanzilishi wa TDC Global
    - Viongozi wa jamii ya kitanzania kwenye mashirika kwenye nchi ambazo ni makazi ya nje ya Tanzania, -na hivyo, hizo jamii zikiandika kuitambua TDC

Global and kusaidia kukuza malengo yake. na watambulike na TDC Global na kuisaidia kukuza malengo yake.

9.KAMATI YA UTENDAJI

Wanachama wa Kamati ya utendaji wa jamii ya ushirika wa kitanzania nchini Sweden watachukua ushiriki wao kwa nafasi moja kwa moja na kusimamia usajili na ushiriki wa kamati ya utendaji ya TDC Global kwa muda wa miaka miwili (2), kipindi ambapo uchaguzi utafanyika kumchagua kiongozi mpya wa baraza kwa mujibu wa masharti ya katiba.

Katika kufanya mabadiliko yoyote ya hapo juu, Timu ya Uongozi itatoa na kuzingatia asili ya uanachama wa kimataifa wa TDC Global, msingi wake, malengo na madhumuni ya kuhakikisha mshikamano wa shirika na uongozi wa mzunguko - bila kukiuka maadili ya sheria ya Chama cha katika nchi husika (ambapo TDC Global imesajiliwa) baada ya uchaguzi utakaofanyika kumchagua kiongozi mpya wa Baraza kwa mujibu wa masharti katika Katiba.

Wanachama waanzilishi wa baraza, wamewekwa kwenye kiambatanishi 4 - yaani **'Orodha ya Wanachama waanzilishi TDC Global'**

Shirika, kupitia baraza, litakuwa na mamlaka zifuatayo:

a) Kuchukua hatua kama vile inaweza kuonekana kuwa sahihi kwa lengo la kufanya malengo makuu / shughuli zilizowekwa hapo juu.

b) Kujishughulisha na malengo mengine mbalimbali zaidi kuliko malengo tajwa hapo juu.

c) Kukuza, kuwa na benki akaunti, kuwekeza, na kutumia mgawanyo wa fedha kwa ajili ya maslahi ya jamii ya ushirika wa watanzania waishio ughaibuni.

d) Kushirikisha washauri na kupokea ushauri ili kufanikisha uhakika na usahihi mara kwa mara.

e) Kuwekeza fedha yoyote ambayo haina ulazima wa haraka kwa shughuli za shirika katika uwekezaji ikiwa kutakuwa na ulazima wa kufanya hivyo (kuondosha na kutofautisha uwekezaji huo).

f) Kushirikiana na mashirika mengine ya sekta hiari, sekta binafsi, biahara, idara na mashirikia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuendeleza jamii ya ushirika wa watanzania waishio ughaibuni.

g) kufanya jambo lolote ambalo linaweza kuwa la haraka au lenye kufaa katika kuendeleza malengo ya baraza.

h) Kupokea ruzuku, michango na legacies of all kind (na kukubali masharti yeyote yatakayoambatanishwa).

i) Kufanya jambo lolote ambalo laweza kuwa muafaka na lifaalo kwa ajili ya kuendeleza malengo ya taasisi.

j) Baraza la diaspora la watanzania litatakiwa kuipatia kila jumuiya za watanzania kupitia baraza la bara, katika umoja wetu, aina ya utambuzi wa kuwepo kwao. Na kukuza mchango wao katika maendeleo ya Tanzania na maendeleo ya ustawi wa watanzania katika nchi mama na nje ya nchi.

10. UANACHAMA/MJUMBE

a. Uanachama upo wazi kwa ajili ya mtu ambaye ni mzaliwa na raia wa Tanzania, ambaye anaishi nje ya nchi ama kwa uraia wa Tanzania au ameasili uraia wa taifa la nchi nyingine ughaibuni.

b. Iwapo mtu mwenye nia ya kuomba kuwa mwanachama basi atahitajika kukubaliana na kufuata katiba ya Baraza la diaspora la watanzania, sheria, taratibu, kanuni na taratibu zilizowekwa na jumuiya hiyo.

c. Kujiunga na gharama za uanachama wa jumuiya hii, ustahiki wa kuwa mwanachama ni lazima awe amekidhi vigezo husika vya jumuiya kama vilivyoorodheshwa hapo chini.

10.1 VIGEZO/SIFA ZA MJUMBE/MWANACHAMA

a) Mjumbe/Mwanachama atatakiwa kulipa ada ya usajili ya kila mwaka katika kiwango kilichokubalika na kuafikiwa na jumuiya husika.

b) Jumuiya za mashirika/taasisi, watu binafsi, wanachama/wajumbe wa kushirikishwa, isipokuwa kwa wajumbe Maalum watalipa ada ya usajili ya kila mwaka na ada ya kujiunga.

c) Wajumbe /wanachama watakaoshindwa kulipa ada zao watazuiliwa kupata mafao yao mpaka malipo ya ada zao yatakapolipwa kwa ukamilifu.

10.2 AINA YA WANACHAMA/WAJUMBE

a) Mjumbe/mwanachama ambaye ni mtu binafsi
b) Wajumbe /Wanachama ambao ni Jumuiya/Taasisi
c) Mjumbe/Mwanachama ambaye ni Shirika
d) Mjumbe/Mwanachama ambaye ni Mtu/Watu maalum

10.3 USTAHIKI / AINA ZA UANACHAMA

Ustahiki wa kila mjumbe/mwanachama huamuliwa kutokana na kila kundi kama ifuatavyo.

a) Mwanachama ambaye ni mtu/watu binafsi

Mwanachama huyu ni mtu binafsi ambaye hajajiunga na jumuiya yeyote ya watanzania katika nchi anayoishi na nchi hiyo iwe nje ya Tanzania.Mjumbe/mwanachama lazima awe anaishi ugenini/ughaibuni.

b) Mwanachama ambaye ni Jumuiya/Taasisi

itakuwa kwa jumuiya zote za wanadiaspora wakitanzania

c) Mwanachama ambaye ni Shirika.

Itakuwa kwa makampuni ama taasisi ambazo zinatoa msaada kusaidia malengo ya TDC Global na/au wafadhili wa kifedha wa shughuli mbalimbali za TDC Global.

d) Mwanachama Maalumu

I. Baraza litaamua juu ya mapendekezo ya wajumbe/wanachama wa baraza husika na shirika, ama;

II. Baraza linaweza kutoa ujumbe/uanachama maalum katika kipindi ambacho litaona inafaa kwa mtu ama taasisi kwa sababu ya umahiri na mchango wao katika kuendeleza malengo ya baraza na katika shughuli za maendeleo ya Tanzania.

III. Makundi yasiyo yakitaaluma na taasisi za kibiashara ambazo zimevutiwa na Tanzania.

IV. Watu binafsi wasio watanzania wanaoishi ugenini ambao wana maslahi na wanatambua nia ya TDC Global na kushiriki maono yake.

V. Wataruhusiwa kuingia kwenye mikutano muhimu na kupata haki ya kujadili, bila kupiga kura.

VI. Wajumbe/wanachama maalum hawafungwi na ulazima wa majukumu/wajibu wa siku hadi siku, ingawa ushauri wao na hoja zao za kitaalam kuhusiana na majadiliano mbali mbali zitakaribishwa na kuhusishwa katika baraza.

Awe ametoa mchango wa heshima kwa jamii na anaweza kuisadia taasisi na jumuiya zake katika kukuza malengo yake, (kuhakikisha hakuna mgongano wa maslahi unatokea, tamko la mgongano wa maslahi lazima lisainiwe.

10.4 Haki na Mafao ya Wanachama

a) Haki ya kuhudhuria na kutoa maoni katika mikutano ya shirika husika.

b) Haki ya kushiriki katika mikutano na shughuli nyingine kama itahusika.

c) Haki ya kuchagua viongozi na haki ya kuchaguliwa kwa mujibu wa Katiba hii, miongozo na taratibu.

d) Haki ya kushiriki katika shughuli za shirika sambamba na utaratibu uliowekwa.

e) Wanachama watakuwa wakifaidika na jitihada za Baraza la kuendeleza maslahi ya Diaspora Tanzania kama ilivyoelezwa katika malengo ya Baraza la hapo juu.

10.5 Kusimamishwa kwa Mjumbe/Uanachama na Kinga.

a) TDC Global itamsimamisha mwanachama yeyote binafsi au shirika lolote ambalo litajihusisha na shughuli yeyote iliyo kinyume na maslahi ya TDC Global. Mwanachama yeyote atakayesimamishwa atakuwa moja kwa moja kasimamishwa katika kutekeleza haki au upendeleo wowote wa uanachama .

b) Kwa si chini ya siku 14 taarifa iliyoandikwa ya kusimamishwa itatolewa na nafasi stahiki ya kuwasilisha kwa baraza wakati likimpatia mwanachama nafasi nzuri ya kusikilizwa au kufanya uwakilishi kuhusu kusimamishwa huko.

Mwanachama anaacha kuwa mwanachama siku 14 baada ya siku ambayo uamuzi huo wa kusitisha uanachama wake umewasilishwa kwake kwa maandishi.

Mwanachama ambaye atakuwa amesimamishwa, kama anataka kukata rufaa dhidi ya kusimamishwa kwake, atatakiwa kutoa taarifa kwa katibu wake kuhusu dhumuni la kufanya hivyo ndani ya siku 14 kama ilivyo hapo juu.

c) Mjumbe/Mwanachama ambaye alitoa taarifa kwamba haachi kuwa mwanachama ila mpaka uamuzi wa Baraza kusitisha kwake imethibitishwa.

10.6 USAJILI WA WANACHAMA.

Katibu wa Baraza la diaspora la watanzania atahifadhi majina na taarifa za mawasiliano ya kila mwanachama katika daftari la wanachama ikiwa ni pamoja na njia ya kielektroniki.

i. Katibu atakuwa na wajibu wa kufanya daftari la wanachama lipatikane kwa ajili ya ukaguzi wakati huo huo akifuata sheria za faragha na kulinda haki ya mtu binafsi ya faragha.

ii. Mwanachama ambaye atabadili taarifa zake za mawasiliano atatoa taarifa kwa katibu moja kwa moja au kupitia kwa kiongozi wake wa jumuiya mama.

iii. Itakapokuwa mjumbe/mwanachama amehama moja kwa moja na hivyo si tena mkazi wa nchi ya ugenini/ughaibuni, atatakiwa kuondolewa kwenye daftari la usajili na hatotakiwa kupata faida na upendeleo isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo

11.BODI YA USHAURI YA BARAZA

TDC Global itaongozwa na Kamati ya utendaji ambayo itasaidiwa na bodi ya ushauri.

11.1Bodi ya ushauri ya baraza la diaspora la watanzania itakuwa na;

a) Timu ya uongozi wa TDC Global, ambayo imeundwa na;

- Wanachama waanzilishi wa TDC Global (Orodha katika kiambatanisho 4)
- Waliochaguliwa na kamati ya utendaji inayowakilishwa na mwenyekiti (Mjumbe mshiriki)
- Viongozi wote wa jumuiya za watanzania katika nchi nje ya Tanzania ambapo wanadiaspora wanaishi na mashirika mengine yote yanayoitambua TDC Global kwa maandishi na kusaidia malengo yake

12. KAMATI KUU YA UTENDAJI

Kutakuwa na kamati kuu ya utendaji ambayo ndiyo chombo cha uongozi ambacho kitaundwa na maafisa waliochaguliwa:

a) Mwenyekiti
b) Naibu Mwenyekiti
c) Katibu
d) Naibu Katibu
e) Mweka Hazina
f) Wanachama wa kamati (wasiopungua watu 6).

12.1 MIKUTANO YA KAMATI KUU TENDAJI

Kamati itakutana angalau mara moja kwa mwaka ana kwa ana na angalau mara mbili ya ziada ama ana kwa ana au kupitia “teleconferencing” au mikutano ya video, na itatumia uwezo wa mamlaka ya utendaji katika hiyo ya mikutano Baraza.

12.2 TIMU YA UONGOZI TDC GLOBAL
Timu ya uongozi wa TDC Global itaundwa na;
Mwenyekiti wa kamati ya utendaji, viongozi wote wa jumuiya/taasisi au ushirika wa wakitanzania ambapo wanadiaspora wanaishi na vile vyama vyote ambavyo vimeitambua TDC Global kama mwakilishi wao na kwamba ndicho chombo cha juu cha wanadiaspora duniani.

12.3 KAZI ZA TIMU YA UONGOZI WA TDC GLOBAL
Timu ya uongozi itaisaidia timu ya utendaji nje ya mikutano rasmi ya kamati ya utendaji wakati itakapohitajika au kwa ombi la kamati ya utendaji.

Kazi za Timu ya Uongozi Itakuwa ni pamoja na:
Utatuzi wa migogoro, makosa kadhaa ya wanachama wa kamati ya utendaji ikiwemo matumizi mabaya ya fedha za baraza,kutatua migogoro mikubwa ya wanachama wa kamati ya utendaji, timu ya uongozi na wanachama wa kawaida ambao wa wanaweza kuletea sifa na heshima kwa baraza, kusimamia mgongano wa maslahi ndani ya TDC Global na masuala mengine yeyote ya kuamuliwa na baraza.

Kutoa msaada kwa kamati ya utendaji na kamati zote za kudumu ambavyo itafaa katika kutimiza maono ya TDC Global na malengo kwa kuchukua hatua zote nzuri na muhimu ili kuhakikisha utawala bora wa ushirika, ikiwa ni pamoja na kuleta mapendekezo kwa kamati ya utendaji na kamati za kudumu ipasavyo.

13. UCHAGUZI WA KAMATI YA WANACHAMA YA UTENDAJI (Pia inajulikana kama Maafisa waliochagulia).

a) Mwanachama yoyote mwenye uwezo wa kifedha anaweza kuchaguliwa na katika uchaguzi kwa nafasi ya afisa yoyote ambaye atachaguliwa na wanachama wa sasa wenye uwezo wa kifedha au yoyote ndani ya jamii ya watanzania au vyama/mashirika ambayo hufadhili wanachama wa shirika na baraza.

b) Uteuzi kwa nafasi zote za uteuzi za afisa zitawasilishwa kwa afisa msimamizi (2) katika kalenda ya miezi kabla ya mkutano husika wa baraza.

c) Uteuzi lazima uonyeshe kwa uwazi jina la mteule, mpendekezaji na mpitishaji, katika nafasi ambayo mtu ameteuliwa na makubaliano yake.

d) uteuzi utaambatana na taarifa kutoka kwa mteuzi sahihi ikiwa watu wote watatu (mteule, mpendekezaji na mpitishaji) ni wanachama wa kifedha wa TDC Global.

e) Maafisa wa kuchaguliwa wa TDC Global watakuwa wamechaguliwa kwa kipindi cha miaka miwili ya kalenda na wanaweza kutumikia zaidi ya vipindi viwili mfululizo katika nafasi yoyote moja wapo. Hakuna mtu anaweza kutumika kama Afisa aliyechaguliwa kwa zaidi ya miaka minne mfululizo.

f) Uchaguzi wa nafasi zote za viongozi ni utafanyika kila baada ya miaka miwili ambapo mfumo huu utaanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2019 katika mkutano mkuu.

13.1 WAJIBU WA WAJUMBE WA KAMATI YA KIUTENDAJI WALIOCHAGULIWA

Mwenyekiti atakuwa:

a) Ndio Kiongozi wa Mikutano Mikuu ya Baraza;

b) Ni wajibu wa mwenyekiti kuhakikisha mikutano hufanyika katika mahali na mazingira mazuri, kuwa mbunifu na mazungumzo yanatakiwa kuwa ya wazi.

c) Kuwa mjumbe mshiriki tu wa kamati zote, mitandao yote na vikosi kazi vya TDC.

d) Kuwa ni Msemaji Mkuu kwa niaba ya TDC Global.

e) Awe na Mamlaka ya kukaimisha madaraka ya kutoa taarifa kwa umma wa wanachama wengine wa kamati ya utendaji.

Mwenyekiti lazima asimamie mambo ya Kamati ya Utendaji ili kuiwezesha

a) Kufanikisha majukumu yake na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa za kutosha na kwa muda muafaka ili kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake;

b) Mwenyekiti ana mamlaka ya kuwakilisha bodi nje ya mikutano;

13.2Kaimu Mwenyekiti akakuwa:

a) Naibu Mwenyekiti atakaimu nafasi ya Mwenyekiti kama ikitokea mwenyekiti hatokuwepo;

b) Kuwajibika katika utendaji kwa ajili ya ufanisi wa kamati zote za TDC Global zilizotolewa katika Kiambatanisho 3.

c) Kumsaidia mwenyekiti na kuwa mjumbe mshiriki wa kamati zote za kudumu na;

d) Kufanya kazi zote zitakazokaimishwa na mwenyekiti au kamati ya kiutendaji ya TDC Global na;

e) Iwapo ikitokea hali ya kutojiweza, kukosekana au kujiuzulu kwa mwenyekiti, Naibu Mwenyekiti atafanya kazi zote za mwenyekiti na kuendelea na majukumu yake yote mpaka Mwenyekiti atakaporejea au Mwenyekiti mpya atakapochaguliwa.

13.3 Katibu atakuwa:

a) Kuandaa Adidu za rejea na ajenda za hoja mbalimbali katika mikutano yote ya baraza na utendaji, ikiwa ni pamoja na majina ya wanachama walio hudhuria pamoja na kurekodi udhuru mbalimbali.

b) Kuhakikisha kuwa adidu za rejea zimesainiwa na Mweyekiti wa mkutano alioongoza au mkutano uliofanyika mbele ya mwenyekiti huyo.

c) Kuhakikisha kuwa taarifa na agenda vinatolewa kihalali kama inavyotakiwa kwa mujibu wa katiba hii.

d) Kuandaa miniti kwa ajili ya uteuzi wote wa viongozi wa ofisi pamoja na wajumbe wa kamati ya utendaji.

e) Kuzitaarifu mamlaka zote husika kuhusu marekebisho ya kikatiba na mabadiliko katika viongozi wa ofisi ya baraza katika muda unaohitajika na kama ilivyo katika taratibu za vyama vya nchi ambayo TDC Global itakuwa imesajiliwa.

Kufanya kazi nyingine, zitakazo kaimishwa na mwenyekiti au kamati ya kiutendaji ya baraza.

f) Kuhakikisha kwamba maombi yote kwa ajili ya uanachama wa Baraza yanapokelewa na kuwasilishwa kwa kuzingatia, na kuhakikisha Daftari la wanachama linaimarishwa na kuhifadhiwa salama na kwa mujibu wa Sheria ya Chama cha bila kukiuka maadili ya sheria za faragha ya mtu binafsi.

13.4 Mweka Hazina atatakiwa:

a) Kuhakikisha kuwa kila fedha zilizokusanywa kutokana na TDC Global zinakusanywa na zinapokelewa.

b) Kuhakikisha kwamba malipo yote yanaidhinishwa na TDC Global yanafanyika.

c) Kuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba vitabu sahihi na akaunti zinaonyesha maelezo ya fedha za mapato yote, risiti na matumizi yanayohusisha shughuli za TDC Global.

d) Kuhakikisha kwamba vitabu vya mahesabu na akaunti vinapatikana kwa ajili ya ukaguzi wa mahesabu pindi vitakavyohitajika.

e) Kuhakikisha kwamba taarifa za fedha na mahesabu, zinakaguliwa kihalali, na kuwasilishwa kwa wanachama kabla ya mkutano mkuu wa mwaka.

f) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwenyekiti au kamati ya Utendaji wa TDC Global.

13.5 NAFASI ZA AJIRA

Ikiwa itatokea nafasi yoyote kwenye kamati ya utendaji au bodi ya uanachama, mweyekiti ataitisha mkutano na kamati ya utendaji kwa ajili ya kushauriana na timu ya uongozi kujaza nafasi iliyowazi na mtu atakayechaguliwa na Mtendaji atakuwa madarakani mpaka mkutano utakaofuata/ujao akiwa na sifa, na anaweza kujitokeza kwa ajili ya uchaguzi, kwa ajili ya kubaki, kama masharti ya kamati ya utendaji ya mwanachama yamebadilishwa.

Nafasi iliyoachwa wazi hutokea katika kamati ya utendaji au Bodi wakati mwanachama wa ofisi hiyo inakuwa wazi kama mwanachama huyo:

a) Amefariki

b) Akijiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi itakayo wasilishwa kwa mwenyekiti, au ikiwa kama mwanachama ni mwenyekiti wa kamati ya utendaji basi kwa naibu mwenyekiti.

c) Akibainika kufanya kosa kinyume cha sheria.

d) Imebainika ana tatizo sugu la kiakili na kimwili.

e) Kutohudhuria mikutano ya kamati ya utendaji au mikutano ya bodi zaidi ya mara (3) katika kipindi cha mwaka huo huo wa fedha

ambapo amepokea taarifa, bila idhini ya kamati ya utendaji au bodi au kutowasilisha taarifa za udhuru wake kwa mwendesha mikutano husika;

g) Kama atakuwa amefirisika au kufanya utaratibu wowote wa kutunga kulipa wadeni wake wote kwa ujumla,

h) Ikiwa atakoma mara moja kuwa raisi/Mwenyekiti wa jumuiya ya watanzania katika nchi ambayo anaishi, kisha nafasi itatakiwa kupiewa mwenyekiti ajaye isipokuwa taratibu zimefafanyika na kukubaliwa na baraza.

14. KAMATI ZA KUDUMU

Kamati ya Utendaji kwa kushauriana na timu ya Uongozi kwa hiari yao wenyewe au juu ya mapendekezo ya wanachama wa baraza wataanzisha kamati za kudumu, mitandao, vyama vya kazi au vikosi kazi vya TDC Global wakati wowote itakapo hitajika ili kutimiza malengo ya baraza. Kamati kuu itakuwa na;

Kamati za Kudumu zitakuwa:

I. Kuwa sehemu ya mpango mkakati na moango kazi ukiangalia masuala yote muhimu ya jamii kama itakavyoanishwa na baraza.

II. Kumchagua mwanachama yeyote wa baraza kwa mnajili huo, mwenye maarifa, utalaam na ujuzi katika maeneo yaliyoainishwa kwa ajili ya kuitumikia kamati ya kudumu wakati huo huo usawa wa kijinsia ukizingatiwa wakati wote.

14 .1 Ushiriki wa kikamilifu wa vijana wa kitanzania katika kamati za kudumu
Inafahaika kwamba idadi ya watu wa Afrika ni zaidi ya bilioni 1.2 na asilimia 60 yawengi wao ni umri wa miaka 30 na chini (2017); na Agenda ya mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika "Lengo 18", limetoa wito wa kuimarisha mgao idadi ya watu kupitia uwekezaji katika vijana, Uongozi wa TDC Global utakuwa;

I. Kuwashirikisha na kuwawezesha vijana wa Tanzania kwa kuhakikisha kwamba uongozi wa baraza linashiriki kikamilifu inahimiza ushiriki kamili wa vijana katika masuala yote ya shughuli za baraza;

II. Kuhakikisha vijana wanahusishwa katika ngazi zote za muundo.

III. Kwa wakati wote kuwa na umakini wa kujiepusha na ubaguzi wa kiumri na kuweka mkazo katika jukumu la vijana wa kitanzania waliopo ughaibuni kuwa sehemu muhimu katika kujenga maendeleo endelevu ya nyumbani.

Kamati za kudumu kwa maana hiyo zitaimarishwa na kuongozwa na ufahamu wa kuwa vijana wa kitanzania ni hazina inayopaswa kuendelezwa kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania.

15. BODI YA WAKURUGENZI
Kamati ya utendaji kwa kushirikina na uongozi wa timu wana mamlaka ya kuanzisha bodi ya wakurugenzi kwa wakati ambao utafaa, wakiona inafaa na kwa mahitaji ya Baraza.

Mkurugenzi Mkuu

Atakuwa na wajibu wa kila utekelezaji wa siku hadi siku wa mipango ya muda mrefu na mfupi ya baraza.Mkurugenzi Mtendaji atahusishwa moja kwa moja kati ya Kamati ya Utendaji, Timu ya Uongozi na timu ya uongozi na usimamizi wa Kamati za Kudumu za TDC Global. Mkurugenzi Mtendaji atakuwa akiwasiliana na Kamati ya Utendaji na Uongozi wa timu ya TDC kwa ajili ya Utekelezaji wa mpango mkakati wa TDC Global, na kusimamia utendaji wa baraza katika kufikia malengo

Wajibu na majukumu ya Mkurugenzi Mkuu Mtendaji

i. Kusimamia uendeshaji wa TDC Global;

ii. Kuunda sera na mapendekezo ya mipango kwa kamati ya utendaji;

iii. Kushauri uongozi wa baraza na ataamua na kuongoza njia sahihi katika uratibu wa shughuli;

iv. Kuitangaza /kuikuza TDC Global duniani kote;

v. Kushauri uongozi wa baraza na ataamua na kuongoza njia sahihi katika uratibu wa shughuli;

vi. Kusaidia kutoa motisha kwa wafanyakazi katika shughuli za TDC Global;

Mkurugenzi mtendaji anatakiwa kuwa mwenye maono au mbeba za baraza. Atatakiwa kutazama fursa za mbeleni katika SHERIA NA SERA YA DIASPORA YA TANZANIA zinazowaathiri wanachama wake, muingiliano wa mabaraza, wajumbe na waajiriwa (kama wapo) na muingiliano baina ya wadau wa mashirika na wanachama.

Kwa ujumla Mkurugenzi Mtendaji atakuwa:

I. Kuweka mbele maamuzi yote ya mikutano ya kamati ya utendaji na kuhudhuria mikutano ya bodi zote (pale bodi inapokuwa imeundwa) na kufuatilia juu ya uekelezaji wa hatua mabazo zinahitaji kufanyika ili kutimiza malengo ya baraza.

II. Kuwasilisha ripoti za mara kwa mara katika uendeshaji wa TDC global katika mzunguko na katika muundo wa kuamuliwa na kamati ya utendaji na kukubaliwa na bodi (mara bodi hiyo itakapokuwa imeundwa na kuanza kufanya kazi kikamilifu).

III. Kuchangia mawazo kwa kamati ya utendaji na masuala yoyote ambayo yanahitaji kuangaliwa.

IV. Kuhakikisha uratibu wa shughuli mbalimbali za baraza zinazofanywa kishirika na muundo katika kamati ya utendaji, timu ya uongozi, kamati ya kudumu na wadau wengine wanaofanya na baraza katika kufikia malengo yake.

V. Kuhakikisha kuwa muhuri wa baraza upo kwenye matunzo salama na kwamba utatumika kwenye matumizi yenye mamlaka sahihi ya mwenyekiti wa kamati ya utendaji.

VI. Kutoa maoni kwa wafanyakazi wengine walioajiriwa na baraza la maamuzi kupitia kamati kuu ya utendaji na bodi inayohusika na huduma hiyo.

17. MKUTANO MKUU

a) Mkutano mkuu wa mwaka utafanyikia sehemu ambayo imechaguliwa na kamati kuu ya utendaji

b) Mikutano ya utendaji itafanyika nchini Uswidi au sehemu yoyote nyingine kama itakavyokuwa imepangwa na kamati ya utendaji baada ya kushauriana na timu ya Uongozi wa TDC Global. na inawezekana ikahairishwa au vinginevyo kwa wakati wowote kama ikibainika kuna sababu zinazofaa.

c) Mwenyekiti anaweza akaitisha wito wa mkutano wa 'kamati kuu' ya utendaji muda wowote au mkutano wa pamoja...mkutano wa pamoja na timu ya uongozi ya TDC Global.

d) Katibu ataitisha ombi la mkutano wa kamati ya utendaji ya TDC Global au kuitisha mkutano wa kamati za kudumu.

e) Katibu atatoa notisi ya si chini ya siku thelathini (30) ya mikutano yote kwa wanachama wa kamati ya utendaji na timu ya TDC Global pamoja na kubainisha mahali , saa na siku ya mkutano ili kuandaa mipango ya mkutano huo.

18. MABADILIKO YA KATIBA

a) Katiba hii inaweza kubadilishwa kwa makubaliano yatakayopitishwa na robo tatu ya wajumbe wateule wa kamati kuu watakaokuwepo na kura zitapigwa kwenye mkutano mkuu wa kila mwaka au mkutano mkuu maalumu, ikiwa tu angalau taarifa ya siku zisizopungua 60 itatolewa juu ya mabadiliko hayo.

b) Mabadiliko ya katiba hayataanza kufanya kazi rasmi mpaka pale nakala ya mabadiliko itakapo idhinishwa na muhuri maalumu wa halmashauri kuwa nakala halisi ya makubaliano yanayoathiri katiba itakapopelekwa kwenye ofisi za vyama zinazohusika na usajili huko Uswidi na ada stahiki kulipwa.

19. SERA

(a) Kabla ya kuanzisha sera yoyote kwa jina la TDC Global, wajumbe wote wa kamati kuu na viongozi wote watajulishwa.

(b) Katika suala ambapo muda wa ushirikishi unahitajika, maelezo yote ya kina na njia za utatuzi zinazotegemewa kuchukuliwa zitawekwa wazi kwa maandishi na mwenyekiti wa kamati ya uongozi na wajumbe wa kulipwa wataainisha muda halisi wa kupokea maoni yao. Baada ya muda uliopangwa kuisha, mwenyekiti ataangalia maamuzi yaliyopitishwa na wajumbe wengi zaidi na maamuzi hayo yatakua ndio maamuzi ya Kamati kuu.

(c) kama hakutakuwepo uwezekano wa kuwafikia wajumbe wote wa kulipwa kwa ajili ya maoni yao, wajumbe wa kamati ya uongozi watataarifiwa kupitia barua pepe, WhattsApp au mawasiliano kwa njia ya skype, na iwapo mawasiliano haya yote hayatawezekana, na iwapo watoa maoni hawajulikani, hakuna hatua yoyote itakayochukuliwa.

20. MWAKA WA FEDHA

Mwaka wa fedha utaisha tarehe 31 mwezi wa 12 kila mwaka, na taarifa ya fedha iliyokaguliwa itawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka unaofuatia.

21. WANACHAMA WAPYA

Gharama za kuomba kujiunga upya kila mwaka kwa wanachama wote zitapitishwa na kamati kuu ya halmashauri kwa kushirikisha kamati ya uongozi.

21. FEDHA NA AKAUNTI

(a) Fedha zote zitakazopokelewa na TDC Global zitaingizwa kwenye akaunti ya benki yenye jina la TDC Global. Miamala yote itakayofanyika ya kupokea/kutoa fedha lazima hati ya malipo/risiti itokewe/zitolewe.

(b) akaunti zote zitawasilishwa kwa kamati kuu ikiwa ni pamoja na maelezo ya kina juu ya akaunti hizo, na maelezo hayo yataingizwa kwenye kitabu cha kumbukumbu za mikutano.

(c)Kiasi chochote cha pesa kilichozidi kiasi kilichokubaliwa na kamati kuu kitalipwa na TDC Global kwa njia za kielektroniki au kwa hundi na kuwekewa saini na watia saini wowote wawili wa akaunti ambao ni mwenyekiti, katibu na mweka hazina.

23. MKAGUZI WA HESABU

Mkaguzi atateuliwa na kamati kuu;

a) Kamati kuu itahakikisha inateua mkaguzi wa hesabu ambaye ana sifa moja kati ya hizi zifuatazo;
b) Awe mkaguzi aliyeidhinishwa na bodi ya wakaguzi, mkaguzi aliyeko katika jumuiya ya wakaguzi au aliyewahi kuwa katika jumuiya ya wakaguzi. Mkaguzi atakua na uhuru na vitabu vya hesabu vya halmashauri kuu na anaweza kukagua taarifa ya fedha ya mwaka.
c) Ili kuonyesha uwazi na ukweli wa taarifa za kifedha za halmashauri kuu katika kila mkutano mkuu wa kila mwaka, mkaguzi haruhusiwi kuwa mjumbe wa halmashauri kuu kwa mwaka wa fedha ambao yeye ni mkaguzi.
d) Mkaguzi haruhusiwi kuwa ofisa wa ofisi yoyote au kuwa na uhusiano wowote na ofisa yoyote wa TDC Global.
e) Mkaguzi hataingiliana na mtu anayesimamia maswala ya kifedha ya kila siku ndani ya TDC Global.
f) Ukaguzi utafanywa mara kwa mara kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili
g) Ikitokea ofisi ya mkaguzi ikawa wazi, kamati kuu itateuwa mkaguzi wa muda mpaka mkutano mkuu utakaofuata.
h) Taarifa ya hitaji la kubadilisha mkaguzi ni lazima ifike kwa katibu angalau siku 21 kabla ya mkutano mkuu wa kila mwaka.
i) Katibu atamtumia mkaguzi aliyepo hati ya mabadiliko hayo angalau siku 7 kabla ya mkutano mkuu wa kila mwaka. Mkaguzi aliyepo atahudhuria mkutano huo mkuu kwa gharama zake mwenyewe, kama atataka kusikilizwa katika mkutano huo.

24. BIMA

TDC Global wakati wote itahakikisha inaweka bima juu ya;

I. Madai ya umma,
II. Fidia za wafanyakazi na
III. Kwa hatari yoyote itakayoonekana hivyo na kamati kuu kwa mujibu wa sheria na kanuni za jumuiya za nchi iliposajiliwa TDC, Uswidi

25. UWAZI WA MASLAHI

a) Mjumbe yeyote wa kamati kuu au kamati ya uongozi ataweka wazi maslahi yake kwenye mkataba wowote au makubaliano yoyote baada ya kuingia kwenye makubaliano hayo na ataweka wazi maslahi yake kwenye mkataba au makubaliano hayo katika kikao cha kwanza kitakachofuatia cha TDC Global.

b) Ikiwa mwanachama wa kamati atavutiwa na mkataba au utaratibu baada ya kuundwa au kuingizwa, mwanachama atatakiwa kuwa wazi na kuwasilisha maslahi yake katika kikao cha kwanza cha baraza la TDC Global.

26. KUFUNGWA NA KUFILISIKA

a) Kama itatokea kufungwa kwa TDC Global, kufungwa huko kutafanywa kwa mujibu wa sheria na taratibu za Uswidi
b) Mchango wa madai ya kila mwanachama utakua kwa kiasi ambacho mwanachama hakumalizia kulipa katika ada ya uanachama wake.
c) Mali zote za TDC Global zitakazokuwepo baada ya kufugwa kwa TDC Global zitahamishiwa kwenye jumuiya yenye malengo sawa na TDC Global iliyosajiliwa chini ya kanuni za jumuiya za Uswidi au katika nchi ambamo jumuiya hiyo mfaidika imesajiliwa.
d) Baada ya kufungwa au kufilisika, itakua ni jukumu la baraza kuhamishia mali zilizobaki za TDC Global kwa jumuiya nyingine yenye malengo sawa na TDC Global.

27. USULUHISHI WA MIGOGORO

Jumuiya itatengeneza sera za usuluhishi wa migogoro na utaratibu wa kufuatwa, na itahakikisha kuwa, zimegawiwa kwa kila mjumbe, maofisa na waajiriwa wa jumuiya.
Hata hivo, kikanuni na iwapo sera tajwa hazitakuwepo, kwa mgogoro wowote utakaotokea chini ya katiba hii, pande zote mbili zitakubaliana kufanya maelewano yenye faida kwao wote.
Na kama hawakuweza kuelewana, wataendelea na usuluhishi katika baraza la usuluhishi kwa kamati ya uongozi ya TDC Global.
Kama bado hakutakua na maelewano, atateuliwa mtu kwa makubaliano ya pande zote mbili asiyehusika kwa vyovyote na upande wowote. Mtu huyu aliyeteuliwa atatakiwa kutoathiri haki stahiki ya pande zote mbili.

28. KANUNI ZA MWENENDO NA MAADILI

Jumuiya itatengeneza kanuni za mwenendo na maadili ambazo zitafuatwa na wanachama wote wa TDC Global, viongozi wa jumuiya, waajiriwa wa jumuiya ikijuimuisha washauri na wakandarasi katika kufanya kazi zaTDC Global au kazi zingine za jumuiya.

29. SHERIA ITAKAYOTUMIKA

Katiba hii imetengenezwa kwa mujibu wa sheria za Sweden na itaendeshwa kwa sheria hizo.

30. UANACHAMA WA MAISHA

Waanzilishi wa jumuiya hii wana haki ya uanachama wa maisha katika kamati ya uongozi. Kamati kuu kwa kushirikiana na kamati ya uongozi wana nguvu ya kutoa uanachama wa heshima ambao hata hiyvo hawatakua na haki ya kupiga kura.

31. MAMBO YAFUTAYO YATAFANYIWA KAZI KATIKA MKUTANO MKUU WA KILA MWAKA;

- Kupitishwa kwa kumbukumbu za kikao kilichopita
- Kupokea taarifa ya mwaka ya mwenyekiti
- Kupitisha taarifa ya mwaka
- Kurejea makubaliano ya kikao kilichopita
- Kupokea taarifa ya mweka hazina na taarifa za kifedha.
- Pa;e inapohitajika, kufanya uchaguzi au uchaguzi wa marudio wa wajumbe wa kamati kuu.

APPENDIX 1

MAELEZO

Mwenyekiti-Mtu aliyechaguliwa katika mkutano mkuu kuongoza kipindi cha miaka miwili. Huyu ndiye msemaji wa kwanza wa jumuiya.

Wajumbe wa kamati kuu wateule- watu waliochaguliwa katika mkutano mkuu kuongoza kipindi cha miaka miwili na wana shughulika na ufanyaji kazi wa kamati kuu ya halmashauri kwenye mikutano mikuu. Wana haki ya kupiga kura kwenye maswala yote ya ndani ya mikutano ya kamati kuu.

Wajumbe wa kamati kuu wateule ni mwenyekiti, wenyekiti wasaidizi wawili (ni lazima angalau mmoja kati yao awe mwanamke), katibu, katibu msaidizi, mweka hazina na wanakamati wengine ambao ni wanachama wa jumuiya, watanzania wanaoishi Sweden.

Mwanachama wakifedha- huyu atakua ni mwanachama mmoja wa TDC Global, jumuiya ya kijamii ya kitanzania, au muunganiko wowote wa wanachama ambao wamelipa ada ya uanachama kwa mwaka kwa TDC Global au kwa mazingira mengine yasiyozuilika, siku moja kabla ya mkutano mkuu.

Mwaka wa jumuiya- Ni miezi kumi na mbili ambayo huisha baada ya mfululizo wa mikutano mikuu miwili.

Mkutano mkuu wa kila mwaka- mkutano mkuu wa kila mwaka wa chama au jumuiya ambao ni lazima ufanyike kabla ya mwezi wa 4 kila mwaka.
Mwaka wa fedha- muda wote kuanzia mwezi wa 1 wa mwaka huo na tarehe 31 ya mwezi wa 12 ya mwaka huohuo.

APPENDIX 2

UTARATIBU WA KUENDESHA MKUTANO MKUU WA HALMASHAURI KILA MWAKA

1. Adidu za rejea za kikao kilichopita ni lazima zisomwe na kuungwa mkono kabla ya majadiliano yoyote kuhusu mambo yatakanayo na taarifa hizo.
2. Wakati wa majadiliano ya mambo yanayotokana na taarifa hizo za kikao kilichopita, kila muuliza swali ana haki ya kuuliza swali moja na maswali mawili ya nyongeza.
3. Hoja yoyote ya kuhitaji ufafanuzi kutoka kwa wajumbe wa mkutano inatakiwa iwe kimaandishi, na iungwe mkono na wajumbe halali wa mkutano, kisha iwasilishwe kwa mwenyekiti wa kikao.
4. Kila hoja inapojadiliwa itajadiliwa mpaka mwisho kabla ya kuendelea kujadili hoja nyingine.
5. Hoja zote zitaanzishwa na kuungwa mkono:
    I. Mjumbe anayeanzisha au kuunga mkono hoja au marekebisho atakua na haki ya kuongea wakati tu wa kuanzisha au kuunga mkono hoja hiyo, na atachukuliwa kama aliyeongea kwaajili tu ya kuanzisha hoja au kuunga mkono hata kama atachangia kwenye majadiliano yatakayofuatia au la.
6. Hoja au marekebisho yoyote baada ya kuwasilishwa kikaoni ina weza isiondolewe bila ruhusa ya kikao.
7. Ikiwa kuna hoja mbili zilizowasilishwa, moja ikidai kwamba jambo fulani litendeke na nyingine ikipinga, hoja chanya ndio itakayowasilishwa kwenye kikao.
8. Kila mjumbe wa kikao atakua na haki ya kuongea mara moja tu kwa kila hoja au marekebisho yake, ukiachilia mbali mleta hoja, ambaye atakua na haki ya kujibu bila kuingiza suala lolote geni.
9. Badiliko moja litafanyiwa kazi baada ya badiliko lingine.
    i. Mleta hoja hana haki ya kujibu
    ii. Mtu mmoja anaweza kuwasilisha mabadiliko zaidi ya moja ikiwa tu kila badiliko linaongelea sehemu zisizofanana za hoja.

a) Mabadiliko yatachukuliwa kwa mpangilio kama yanavyoathiri hoja.
b) Badiliko ni lazima liendane na hoja.
c) Mtoa hoja ana haki ya kujibu. Mtoa hoja si lazima atoe mabadiliko lakini anaweza kuongelea mabadiliko yote bila kuathiri haki yake ya kujibu, hii hujumuisha, majadiliano baada ya kutumia haki yake ya kuongea.
d) Baada ya kuingizwa mabadiliko yote, yaliyowasilishwa na yale yaliyoungwa mkono, itawekwa hoja ya awali ikiwa na marekebisho yote.
e) Ni lazima masikilizano yawepo na yaainishwe bayana, na majadiliano yatakua baina ya mleta hoja ya usikivu na mwenyekiti wa kikao.

f) Hoja za utaratibu wa kutumika zitawasilishwa na kuungwa mkono na wajumbe.
g) Utaratibu ufuatao waweza kuwasilishwa, kupokelewa, na kuwekwa mkutanoni wakati wa kujadili hoja ya msingi:
    i. Kuomba ruhusa ya kubadilisha au kuondoa hoja
    ii. Kwamba suala fulani sasa lianzishwe
    iii. Kuendelea na jambo lingine
    iv. Kuahirisha majadiliano
    v. Kuhamishia jambo hilo sehemu nyingine
    vi. Kujadili nini kifanyike kwa mjumbe aliyetajwa na mwenyekiti
    vii. Kuongeza muda
    viii. Kwamba hoja au mawasiliano yawekwe mezani
    ix. Kuwa kamati kuu
    x. Kuigawanya hoja

Majukumu na haki za mwenyekiti

a) Mwenyekiti ana haki ya kujadili lakini kwanza atamkaimisha mwenyekiti msaidizi, na hatarudi katika kiti cha mwenyekiti mpaka pale hoja itakapojadiliwa na kuisha.

b) Ni kazi ya mwenyekiti kutunza usikivu ili mambo yaende kama yalivyopangwa na na kuwawajibisha waongeaji wanaoenda kinyume na amri/utaratibu waweze kuwa wasikivu.
c) Ikiwa mjumbe ataendelea kurudiarudia hoja au kuelezea mambo yasiyohusiana na hoja, mwenyekiti atamjulisha juu ya jambo hilo na kumzuia kuendelea kuzungumza..

d) Mwenyekiti anaweza kumtaja mjumbe kuwa mvunjifu wa kanuni na wajumbe wote wa mkutano kwa pamoja wataamua nini kifanyike.

e) Kama uvunjifu wa kanuni ukitokea, mwenyekiti ana haki ya kuahirisha mkutano mpaka muda na mahali patakapochaguliwa, na baada tu ya mwenyekiti kutoka katika kiti chake, mkutano utakua umeahirishwa rasmi.

e) Ikiwa wajumbe wawili watataka kuongea kwa wakati mmoja, mwenyekiti ataamua ni nani aongee wa kwanza.

f) kwa kuzingatia muda uliokubalika wa majadiliano juu ya hoja na utaratibu wa kufuatwa, mwenyekiti hataweka hoja mezani ikiwa kuna mjumbe ambaye hakupata nafasi ya kuongea na atataka kuongea. Kama muda wa majadiliano ya hoja hiyo utaisha, mwenyekiti atamruhusu mjumbe anayeongea kumalizia hoja yake, kumruhusu mleta hoja kujibu maswali na kisha ataweka mezani hoja nyingine.

KUPIGA KURA

i. Bila kuathiri utaratibu wa kupiga kura uliowekwa na katiba hii:
ii. Kura zote za awali zitapigwa kwa kunyoosha mikono
iii. Angalau watu wawili watateuliwa na mwenyekiti kuhesabu kura, na hesabu za kura zilizoshinda au kushindwa zitatangazwa na mwenyekiti na kuandikwa katika kumbukumbu za kikao.
iv. Wajumbe wote wana haki ya kuomba udhuru na utaandikwa kwenye kumbukumbu za kikao.
v. Wingi wa kura huhesabiwa kuwa kura nyingi zimepigwa zikiunga mkono hoja zaidi ya zile zinazopinga.

APPENDIX 3

ORODHA YA KAMATI ZA UTENDAJI

Baraza litatengeneza hadidu za rejea zitakazotumika kwa kila kamati na idara ili kupelekea ufanisi wa utendaji kazi.

1) Kamati ya mahusiano.

- Afisa wa Mahusiano kwa Umma.

2) Kamati ya Tehama na Mitandao ya kijamii.

- Mratibu wa TEHAMA

3) Kitengo cha Biashara cha Baraza

4) Kamati ya uwekezaji na Uchumi

5) Kamati ya Masuala ya Wazee

6) Kamati ya Masuala ya Vijana

7) Kamati ya masuala ya Wanawake

8) Kamati ya masuala ya ustawi wa jamii

9) Kamati ya Maendeleo na kukuza taaluma uvumbuzi na ujuzi

10) Kamati ya kutunisha mfuko wa Baraza

APPENDIX 4

ORODHA YA KAMATI KUU NA WAASISI

1. Abraham Laizer (Norway)
2. Alex Minja (South Africa)
3. Abrahamu Sangiwa (UK) Co - Founder
4. Andrew Mhella (Italy)
5. Ben Kazola (Dallas USA) Co - Founder
6. Bupe Amon Kyelu (Australia NT)
7. Tengo Kilumanga (Sweden) Co – Founder
8. Dr Casta Tungaraza (Australia) Co - Founder
9. Fortunatus Bandu (Denmark)
10. Gerlad Lusingu (UK)
11. Hassan Nganzo (Norway) Co - Founder
12. Jeff Msangi (Canada) Co - Founder
13. Johanes Rwazo (Holland)
14. Kayu Ligopora (Greece)
15. Lambert Tibaigana (Houston USA)
16. Louis Nyalifa (Dubai)
17. Leslie Benjamin (Uganda)
18. Mgaya Maumba (Thailand)
19. Maulid Kagutta (Italy) Co - Founder
20. Morerd Mwakajumba (Australia QLD)
21. Mona Hassan (Australia WA)

22. Norman Jasson (Sweden) Co-Founder
23. Othmar Mwambe (Japan)
24. Shaaban Yusuf Mlongakweli (Turkey)
25. Adolf Makaya Nyagabona (Sweden)
26. Joe Warioba (UK)
27. Neema Kitilya (UK)
28. Dr Donarld Mlewa (UK)
29. Seynab Haji (Sweden)
30. Lucas Mukami (USA DC) Co – Founder

WAJUMBE WA KAMATI YA BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA

31. Proff Marry Masafu (South Africa)
32. Ally Stambuli (Norway)
33. Hamisi Miraji Simba (Turkey)
34. Daddy Hassan (Norway)
35. Sam Temu (USA)
36. Abdulrahman Ally (Italy)
37. Apatae Fatacky (Zimbabwe)
38. Nambiza Namgambwa (Brazil)
39. Idd Sandaly (USA)
40. Jamilah Nurdine (Japan)
41. Adam Taje (Germany)

42. Viola Mbise (USA)

43. Zuhura Mkwawa (UK)

44. Shaban Kachua (Canada)

45. Peter Mfundo (Germany)

46. Daudi Mayocha (USA)

47. Dr Binamu Agustino (Canada)

48. Samuel Bumaku (Canada)

49. Stephen Mseka (Zimbabwe)

50. Rodrick Shao (USA)

51. Tambwe Tumba (Danmark)

52. Mariam Abbas Juma (Thailand)

53. Vera Teri (USA)

54. Fatuma Tandika (Italy)

55. Taki Mussa (Holland)

56. Ally Juma (Germany)

57. Ally Shomary (Dubai)

58. Andrew Matemba (Canada)

59. Abdullah Mandari (Australia)

60. Dr Eileen Mshana (Holland)

61. Dr Julius Hingira (UK)

62. Grace Kijuu (Uganda)

63. Mvula Tiffan (Australia)

64. Begum Razafinjatovo (Belgium)

65. Wilson Mutabazi (UK)

66. Lynne Kimario (UK)

67. Jonas Singo (Norway)

68. Mohamed Semboja (Norway)

69. Abdallah Choba (Turkey)

70. Mubelwa Bandio (USA)

71. Barack Mwaijande (USA)

72. Athuman Mlinga (Mozambique)

73. Charles Lwanda (Australia)

74. Costa Mkama (Ukraine)

75. Criss Solomon (Cuba)

76. Daniel Saul (Sweden)

77. David Mwasha (Belgium)

78. Dulla Matongo (Finland)

79. Fadhiya El-Elhosyn (UK)

80. Fatuma Ndaro (USA)

81. Gasper Ndabi (Belgium)

82. Gerry Mshana (USA)

83. Halima Mwevi (Italy)

84. Job Hans (USA)

85. Joseph Katala (Canada)

86. Jully Dominic (Brazil)

87. Karim Abdallah (Turkey)

88. Leybab Mdegela (UK)

89. Kennedy Jeremiah (USA)

90. Mohamed Kissoky (Luxembourg)

91. Liberatus Mwang'ombe (USA)

92. Gabriel Masanyiwa (Italy)

94. Mercy Maleku (Australia)

95. Mohamed Yango (Finland)

96. Msafiri Kiswaga (Australia)

97. Mshana Masha Mshana (Uganda)

98. Nasser Mnondwa (Italy)

99. Pauline Nzengula (UK)

100. Phesto Enock Mwakyusa (Finland)

101. Sabrina Jensen (Danmark)

102. Samuel Bumaku (USA)

103. Seraphine Bakirale (Australia)

104. Sofia Batarihaya (Italy)

105. Stan Chambe (Rhode Island USA)

106. Sunday Shomary (USA)

107. Sylvana Lubuva (Holland)

108. Tambwe Tumba (Danmark)

109. Victor Mashamba (UK)

110. Dr Hamza Mokiwa (South Africa)

111. Bunduki Bunduki (Austria)